

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO



SHULE YA SEKONDARI NGALEKU
S.L.P. 130
MKUU ROMBO
TAREHE: 14/12/2020

Kumb. Na. NGSS/JS/10/17

Mzazi/Mlezi/Mfadhibili wa

Mwanafunzi:

S.L.P.

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NGALEKU WILAYA YA
ROMBO MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021**

1.0 Utangulizi

Ninayo furaha kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kijiunga na kidato cha **KWANZA** katika Shule ya Sekondari Ngaleku mwaka **2021**. Shule ya Sekondari **NGALEKU** iko katika kijiji cha Ubetu, Tarafa ya Usseri, Wilaya ya Rombo, Mkoa wa Kilimanjaro umbali wa kilometra moja kutoka barabara ya lami ya Moshi - Tarakea. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** ndani ya siku saba.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

Shule hii ni ya kutwa, yaani wanafunzi wanasoma na kurudi nyumbani kwao; kwa hiyo mzazi/mlezi lazima kuzingatia yafuatayo:

- Kwamba mwanao anapata mahali pazuri pa kulala na penye usalama wakati wote akiwa anasoma hapa.
- Jukumu la kuwalea wanafunzi ni letu sote – walimu na wazazi/walezi. Mzazi/mlezi unapoitwa shulenii kuhusu tabia, mwenendo na maendeleo ya mwanao tafadhalii **FIKA** mara moja. Kushindwa kuitikia wito wa shule kunaweza kumsababishia mwanao kurudishwa nyumbani hadi utakapoitikia wito.
- Mwanafunzi akishaingia shulenii atalazimika kushiriki katika shughuli zote za shule bila kujali matakwa ya mzazi/mlezi. Kama mzazi/mlezi atamzuia mwanae kushiriki katika shughuli yoyote ya shule, mwanae anaweza kuondolewa shulenii.
- Mzazi/mlezi toa taarifa shulenii haraka iwapo mwanao ameshindwa kuhudhuria shule.
- Adhabu zitakazotolewa kwa wanafunzi wakosaji ziheshimiwe na zisiingiliwe na wazazi/walezi.
- Pamoja na kwamba mwanao atalala nyumbani (nje ya shule), bado atahesabika ni mwanafunzi wa shule hii mpaka amalizapo masomo. Uongozi wa Shule hautasita kumchukulia hatua mwanao kwa kitendo chochote cha utovu wa nidhamu hata kama kimefanya nje ya shule. Mwanao atabaki kuwa ni mwanafunzi **WAKATI WOTE**, akiwa shulenii au nyumbani kwako.

2.1 Sare za Shule

2.1.1 Wavulana

- (i) Sare ya shule hii kwa wavulana ni suruali mbili za rangi ya "**KIJANI KIBICHI**" zenye marinda mawili na ziwe zimepindwa kwa chini yaani zwe na "Turn up" na zisibane miguuni (upana miguuni usipungue inchi 15).
- (ii) Mashati mawili meupe ya mikono mifupi ya urefu wa kutosha kuchomekea

- (iii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye soli fupi. (Raba mabuti au viatu vya wazi haviruhusiwi).
- (iv) Soksi nyeusi jozi mbili au zaidi
- (v) Mkanda wa uvalia suruali ni mweusi wa ngozi
- (vi) Sare ya michezo ni viatu vya raba, bukta moja ya rangi ya bluu, fulana (T-shirt) ya rangi ya bluu

2.1.2 Wasichana

- (i) Sare ya shule hii kwa wasichana ni sketi mbili za rangi ya “**KIJANI KIBICHI**” zenye urefu wa kutosha
- (ii) Mashati mawili meupe ya mikono mifupi
- (iii) Viatu vya vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye soli fupi. (Raba, “sendo” au viatu vya wazi haviruhusiwi).
- (iv) Soksi nyeupe jozi mbili au zaidi – zisiwe na mapambo ya aina yoyote
- (v) Rangi ya Hijab ifanane na sare ya shule
- (vi) Sare ya michezo ni viatu vya raba na traksuti ya bluu,

NB: Ili kuepuka kutofautiana kwa rangi na mitindo ya mishono, sare ya shule yaani mashati, suruali, sketi na sweta zitashonwa mahali pamoja na mafundi/wazabuni watakaoteuliwa siku ya kikao cha wazazi.

2.2 Vifaa vya masomo

- (i) Daftari 10 kubwa (counter book)
- (ii) Daftari 10 ndogo kwa ajili ya mazoezi/majaribio
- (iii) Kalamu za wino wa bluu au mweusi, rula ndefu na penseli
- (iv) Mkebe wa hesabu (Mathematical set).
- (v) Kamusi ya Kiswahili Sanifu na Kamusi ya Kiingereza.
- (vi) Vitabu vinavyohusiana na masomo ya Sekondari.
- (vii) Mfuko (School Bag) kwa ajili ya kubebia daftari, vitabu na vifaa vingine vya masomo.
Mifuko ya aina nyingine hairuhusiwi.

2.3 Vifaa vya chakula

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na vifaa vyake mwenyewe vya chakula – **sahani, kibakuli, kikombe na kijiko – visiwe vya plastiki au vya kuvunjika (viwe vya aluminium/bati)**

3.0 KABLA YA KUJA HAPA SHULENI UNASHAURIWA KUFANYA YAFUATAYO:

- (a) Jaza ‘Form A’ ya uthibitisho wa afya yako. Fomu hiyo ijazwe na Mganga wa Hospitali Kuu ya Wilaya au Kituo cha Afya kinachotambulika rasmi na Serikali. (**WASILISHA RISITI YA MALIPO YA VIPIMO**)
- (b) Jaza ‘Fomu B’ ya makubaliano ambayo imeambatanishwa.
- (c) Jaza ‘Fomu C’ ya maelezo binafsi yamwanafunzi.
- (d) Soma sheria za shule ambazo zimeambatanishwa.
- (e) Nunua vifaa vyote vya shule ambavyo vimeainishwa.
- (f) Fomu zote zilete shulenii siku ya kuripoti
- (g) Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shulenii akiwa na mzazi/mlezi wake

4.0 MAKOSA YATAKAOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE


- (a) Wizi
- (b) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
- (c) Kugoma na kuhamasisha mgomo
- (d) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
- (e) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu ye yote yule
- (f) Kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shulenii
- (g) Kufuga ndevu
- (h) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
- (i) Uvitaji wa sigara
- (j) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa

- (k) Kupata ujauzito au kutoa mimba
- (l) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
- (m) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
- (n) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
- (o) **Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule**
- (p) Kudharau Bendera ya Taifa
- (q) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
- (r) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi,

MWISHO

Ninachukua fursa hii kukupongeza tena kwa mwanao kuchaguliwa kujiunga na masomo ya Sekondari katika shule hii. Ni matumaini yangu kuwa atatumia fursa hii kwa makini kwa ajili ya manufaa yake na Taifa kwa ujumla. Ninakukumbusha tena kuwa mwanao anatakiwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zote za shule na za nchi wakati wote atakaokuwa hapa shuleni na nje ya shule. Shida zote zipitie kwa walimu wa zamu au walimu walezi wa madarasa na wengineo kutegemeana na shida au tatizo husika, hatimaye ngazi nyingine zifuate kama utatuzi utakuwa haujakamilika.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NGALEKU


GIREON SALEMA VITALIS
MKUU WA SHULE

*MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI
NGALEKU*

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia mingoz yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni zote zilizoordheshwa hapa chini pamoja na nyngine zitakazofafanuliwa kwako baada ya kuripoti shulen. Zote hizi zinalenga katika malezi na madhumuni ya kumwezesha mwanafunzi kuwepo shulen kwa mujibu wa maadili ya Taifa. Kila mwanafunzi anatakiwa kuzisoma kuzielewa na kuzitii sheria zote za shule kama zilivyo pamoja na mabadiliko yatakayotokea mara kwa mara.

Shulen ni mahali pa malezi ya vijana; na katika Taifa hili wanafunzi wote ni lazima waoneshe heshima na adabu kwa wakubwa na viongozi wa aina zote bila kujali kama ni walimu au watu wengine – shulen au nje ya shule. Aidha wanafunzi ni lazima wajiheshimu na kuheshimiana wenyewe kwa wenyewe bila kujali umri, kidato au hali.

Kila mwanafunzi anapaswa kutumia juhud na maarifa katika shughuli aifanyayo kwa manufaa yake binafsi, shule na Taifa kwa ujumla. **Juhudi** ni jitihada katika kufanya kazi na shughuli zote kwa bidii na nguvu; na **maarifa** ni matumizi mazuri ya akili katika kutanzua mambo.

Kila mwanafunzi ni lazima azingatie yafuatayo kwa muda wake wote atakaokaa hapa shulen:

HESHIMA NA ADABU

1. Mwanafunzi ni lazima aoneshe heshima kwa wakubwa na viongozi wote.
2. Mwanafunzi anapozungumza na mkubwa au kiongozi wake ni lazima asimame kwa adabu na awe mtulivu. Ni kosa kwa mwanafunzi kuzungumza na mkubwa wake au kiongozi wa aina yoyote akiwa ameweka mikono mfukoni, anayumbayumba au kuegemea vitu kama vile meza, kiti au ukuta.
3. Kama utakuwa umekaa chini na mkubwa au kiongozi anapita karibu yako ni lazima usimame sawa na kuamkia.
4. Uwapo darasani na mwalimu au kiongozi mwingine ye yeyote akaingia, lazima usimame bila makelele na kuamkia.
5. Mwanafunzi anapoitwa na mwalimu au kiongozi yeyote, ni lazima atembee kwa haraka na kwa ukakamavu. Asingojee kuitwa mara mbilimbili au kufuatwa.
6. Mwanafunzi anatakiwa kuwa mtiffo kwa walimu, wafanyakazi wasio walimu, viranja wa shule na viongozi wake wengine wote. Ni kosa kwa mwanafunzi kukataa kutekeleza mambo anayoagizwa na viongozi wake.
7. Mwanafunzi anatakiwa kuonesha heshima kwa Chama kinachotawala., Serikali, Wimbo wa Taifa, Nembo ya Taifa Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Taifa, fedha ya nchi (sarafu na noti) na Wimbo wa Shule.
8. Mwanafunzi anatakiwa awe na heshima katika hadhara za mikutano, madarasani, sehemu za kulia chakula na sehemu za mikusanyiko rasmi ndani na nje ya shule.
9. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu viranja wote wa shule waliochaguliwa kwa mujibu wa sheria bila kujali kidato au umri. Kumdharaau au kutomtii kiranja ni kuwadharau walimu waliomkabidhi madaraka na wanafunzi waliomchagua. Viranja wanafanya kazi kwa niaba ya walimu na kwa ajili ya wanafunzi wote.

KAZI NA KUWAHI

10. Ni lazima kila mwanafunzi kuwahi katika kila wito unaomhusu.
11. Unatakiwa kuwahi mara zote kufika shulen na kuzingatia ratiba ya shughuli za kila siku kuhusu vipindi nya taaluma, kazi za mikono na michezo, na usikose kutekeleza unavyopangiwa.
12. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwasili hapa shulen kwa siku zote za masomo saa 1:00 asubuhi na kuondoka saa 10:30 jioni. Kutoka nje ya mipaka ya shule kabla ya muda huo ni lazima kuwa na kibali cha Mwalimu wa zamu. Hii ni pamoja na siku nyngine atakazohitajika shulen kwa mujibu wa ratiba.
13. Kazi ni sehemu ya elimu; kwa hiyo utegaji na uzembe kamwe havitavumiliwa.
14. Kila mwanafunzi anapaswa kutumia juhud na maarifa katika kila shughuli halali aifanyayo.
15. Kila mwanafunzi ni lazima ashiriki katika masomo na kazi za mikono. Uzembe, utegaji na utoro wakati wa vipindi nya darasani au kazi za nje/mikono ni kosa kubwa.
16. Wakati wa masomo ikiwa ni pamoja na vipindi nya dini na vipindi nya kujisomea (Private studies), wanafunzi wote wanatakiwa wawe madarasani mwao bila makelele wala kutembeatembea. Kupiga kelele au kutembeatembea wakati wa vipindi nya aina hiyo ni kuwanyima wengine haki yao ya kutumia muda waliopewa.
17. Kujificha mahali popote wakati wengine wakiwa madarasani, kazini, michezoni au mstarini ni makosa.
18. Ni kosa kutofika (kutohudhuria) shulen siku za masomo, au kuondoka (kutoroka) kabla ya muda uliopangwa.

KUTUNZA VIFAA NA MALI

19. Vifaa vyote vinavyotumiwa hapa shulen ni **MALI YA UMMA**. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuhakikisha kwamba vifaa vyote nya shule vinatumika kwa uangalifu na ubanifu; kwamba haviibiwi, haviharibiwi wala kusambazwa katika sehemu ambazo si zake.

20. Ni kosa kwa mwanafunzi kuiba au kuharibu kifaa chochote cha shule au cha mwenzake kama vile kitabu, daftari, dawati, kiti, meza, ndoo, jembe panga n.k.
21. Ni kosa kuandika maandshi ya aina yoyote kwenye milango, kuta, madirisha, meza, viti, madawati n.k.

USAFI

22. Kila mwanafunzi anatakiwa awe msafi wa mwili wake, mavazi, vifaa vyake anavyotumia, maeneo anamokaa – shulenii na nyumbani, matendo yake, mwenendo wake, lugha yake na tabia yake kwa ujumla.
23. Ni kosa kwa mwanafunzi kutoshiriki katika shughuli za usafi wa mazingira kama atakavyopangiwa na viongozi na uongozi wa shule.
24. Sare ya shule itavaliwa wakati wote mwanafunzi atokapo nyumbani kuja shulenii na wakati wote mwanafunzi awapo katika vipindi shulenii kama ratiba ya kila siku inavyoonesha. Vilevile sare ya shule itavaliwa wakati wa ziara za kielimu na mikutano rasmi na wakati wa kurudi nyumbani.
25. Uvaaji wa kihuni, mavazi yasiyostahili, kofia, mikufu, hereni, bangili pete, kufuga ndevu, kucha, kutumia marashi, dawa za nywele, rangi za kucha midomo, nyusi na unyoaji nywele kihuni ni marufuku kwa mwanafunzi.
26. Ni kosa kwa mwanafunzi kutupa karatasi, takataka na uchafu mwingine ovyo. Karatasi, takataka na uchafu mwingine vitupwe jalalani na kuchomwa moto mara moja.
27. Ni kosa kuona na kupita karatasi, takataka na uchafu mwingine bila kuokota na kupeleka mahali pake na kuchoma.
28. Ni kosa kwa mwanafunzi yeyote kutoa visingizio vya uongo.
29. Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea vilabu nya pombe, majumba ya starehe, wala nyumba za kulala wageni (guest houses).
30. Mwanafunzi haruhusiwi kushiriki ulevi wa aina yoyote ile kama vile pombe, bangi, sigara, mirungi na madawa yoyote ya kulevyaa. Vilevile hairuhusiwi kufanya biashara ya vitu hivyo.
31. Ugomvi na matusi ni haramu kwa mwanafunzi – ndani na nje ya shule.
32. Urafiki wa kimapenzi uwapo mwanafunzi hauruhusiwi.

KUFUKUZWA SHULE (Mwanafunzi atakayepatikana na makosa yafuatayo hatavumiliwa – atafukuzwa shule mara moja)

33. Kutohudhuria shulenii kwa muda mrefu (utoro)
34. Kutoka nje ya shule bila ruhusa – utoro wa vipindi na kazi nyingine za nje.
35. Kashfa ya aina yoyote kwa Taifa na viongozi wa Taifa kama vile kudharau Bendera ya Taifa na Viongozi wa Chama Tawala na Serikali.
36. Wizi wa aina yoyote.
37. Kuharibu mali ya Shule au ya umma.
38. Kuoa au kuolewa ukiwa mwanafunzi.
39. Uasherati na ubakaji.
40. Kupata mimba au kumpa msichana mimba.
41. Kutoa mimba, kusaidia kutoa mimba au kujaribu kutoa mimba.
42. Kupigana au kumpiga mwanafunzi, mlezi, au mwanaajumuiya wa shule au jirani.
43. Kuendesha vikao visivyo halali, kuchocha ghasia au migomo shulenii na nje ya shule au kushiriki katika mgomo.
44. Kufanya/kushiriki maandamano ya aina yoyote bila kibali.
45. Kugoma adhabu.
46. Ulevi wa aina yoyote – pombe, sigara, bangi, madawa ya kulevyaa.
47. Kuendesha magendo au ulangazi wa aina yoyote ile.
48. Kucheza kamari.
49. Kosa lolote la jinai litakalothibitishwa na polisi na kufikishwa mahakamani.
50. Kuwa na simu shulenii.

NB: Si lazima kila jambo mwanafunzi aelekezwe. Mwanafunzi anatakiwa kutumia akili na busara kutenda lile linalokubalika na jumuiya ya shule na Taifa kwa ujumla.

FORM A

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by a Medical Officer in a Government Hospital in respect of all new entrants to Ngaleku Secondary School

Full name:

Age:

Please examine the above named pupil as to his/her fitness to study in this school.

1. 'AIDS' test:
2. Blood count (red and white)
3. Eyesight:
4. Hearing:
5. T.B. test:
6. Spleen:
7. Abdomen:
8. Stool examination:
9. Urine examination:
10. Syphilis test:
11. Additional information or any physical, mental, hereditary infection/diseases:

Treatment after examination (Please state nature of treatment)

.....
.....
.....

MEDICAL CERTIFICATION

I have examined the above named boy/girl and consider that he/she is fit/unfit to pursue secondary education.

Signature: Designation:

Station: Date:

FORM B

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**

HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO

SHULE YA SEKONDARI NGALEKU

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2019

Fomu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi pamoja na mwanafunzi aliyechaguliwa kuingia kidato cha kwanza kisha mwanafunzi ailetu shulen. (Ithibitishwe na Afisa Mtendaji wa Kata)

1. Mimi (majina matatu kamili ya mwanafunzi) kwa hiari yangu mwenyewe ninaikubali nafasi niliyopewa ya kuingia Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari Ngaleku. Nitakuwa tayari kuzifuata sheria zote za shule wakati wote niwapo shulen. Kuvunja sheria za shule nitakuwa nimekiuka ahadi hii ninayotoa na ninastahili kuchukuliwa hatua za kinidhamu zinazostahili.

Sahihi ya Mwanafunzi: Tarehe:

2. Mimi (majina matatu kamili) Mzazi*/Mlezi* wa ninaikubali nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda wote awapo shulen analazimika kufuata sheria za shule na kuwa mtii kwa walezi wake. Pia nikiwa Mzazi*/Mlezi* wake ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi yake na kwamba nitamlipia gharama zote zitakazomwezesha kusoma bila kipingamizi wala kisingizio chochote.

Sahihi ya Mzazi*/Mlezi*: Tarehe:

Namba ya simu:.....

3. Mimi Afisa Mtendaji Kata ya ninathibitisha kuwa Ndugu ni mzazi*/mlezi* wa mtoto huyu aliyechaguliwa kujeungwa Kidato cha Kwanza Shule ya Sekondari Ngaleku. Nimeshauriana naye kuhusu wajibu wake kwa mwanaye na amekiri kutimiza wajibu ipasavyo.

Saini ya Afisa Mtendaji Kata: Tarehe:

Muhuri:

*Futa isiyohusika

FOMU C
(FOMU HII IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI)

Mimi
(*jina la mwanafunzi*) nimezisoma sheria za shule na kuzielewa na niko tayari kuzifuata
Sahihi tarehe

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI.....
2. MAJINA MATATU YA MZAZI/MLEZI.....
3. ANUANI YA NYUMBANI:
 - (i) Kijiji:
 - (ii) Kitongoji:
4. TAREHE Y'A KUZALIWA (*mwanafunzi*)..... MAHALI ULIPOZALIWA
- WILAYA..... TARAFU KATA
5. SHULE YA MSINGI ULIPOTOKA.....
6. DINI YAKO
7. UTAIFA: MTANZANIA/SI MTANZANIA:.....
8. JAMAA KATIKA FAMILIA YENU
 - (i) JINA LA BABA
 - HAI/AMEFARIKI.....
 - (ii) JINA LA MAMA
 - HAI/AMEFARIKI.....
 - (iii) JINA KAMILI LA MLEZI (KAMA HANA MZAZI).....
 - (iv) UHUSIANO NA MLEZI.....
 - (v) ANWANI YA MZAZI/MLEZI.....
 - (a) Kijiji:
 - (b) Kitongoji:
 - (c) Namba ya simu.....
 - (vi) KAZI YA BABA/MLEZI (MKULIMA/MFANYAKAZI/MFANYABIASHARA).....
 - (vii) KAMA NI MFANYAKAZI, KAZI YAKE.....
 - (viii) KAMA NI MKULIMA, ZAO MUHIMU ANALOTEGEMEA.....
 - (ix) KAMA NI MFANYABIASHARA, BIASHARA YAKE.....
 - (x) JAMAA KATIKA FAMILIA
 - (a) IDADI YA KAKA
 - (b) IDADI YA DADA.....
 - (c) YEYE NI WA NGAPI KATIKA FAMILIA?
 - (xi) AFYA YAKE.....

.....
Mimi (*mwanafunzi*)

NATHIBITISHA KUWA TAARIFA ZILIZOJAZWA HAPO JUU NI ZA KWELI

(*Sahihi ya mwanafunzi*)

Mimi (*mzazi/mlezi wa wanafunzi*)
NIMEHAKIKISHA KUWA TAARIFA ZILIZOJAZWA HAPO JUU NI ZA KWELI, NA NINAKIRI KUKUBALIANA
NA SHERIA, TARATIBU NA KANUNI, NA KWAMBA NITAMPATIA MWANANGU MAHITAJI YOTE MUHIMU
YA SHULE NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE KATIKA VIKAO VYA WAZAZI

Sahihi ya mzazi/mlezi *Tarehe:* *Namba ya Simu:*